# MTAZAME NYOKA ILI UISHI

## Masomo Kutoka kwenye Hadithi ya Agano la Kale kuhusu Nyoka ya Shaba

BILL PINTO

## MTAZAME NYOKA ILI UISHI

Hadithi yetu inaanzia kwenye jangwa la Misri. Hapa, wana wa Israeli kwa mara nyingine tena walikuwa wanamuasi na kumlalamikia Mungu. "Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka Nchi ya Misri, ili tufe jangwani?" Kitabu cha Hesabu 21:5.

Katika hatua hii, wana wa Israeli walikuwa njiani kuelekea Kanaani baada ya kukombolewa kimiujiza kutoka kwenye utumwa wa Wamisri. Badala ya kuthamini baraka ambazo Mungu alikuwa amewapa, Waisraeli walikuwa na roho ya kutoridhika. Matokeo yake wakakaripiwa juu ya roho hii, "BWANA akatuma nyoka za moto kati ya watu, wakawauma, watu wengi wakafa." Kitabu cha Hesabu 21:6.

Baada ya karipio hilo lenye kutisha kutokana na hasira ya Mungu, Waisraeli walimuomba Musa.

"Tumefanya dhambi," walisema, "kwa sababu tumemnung'unikia Mungu, na wewe; utuombee kwa BWANA, atuondolee nyoka hawa." Mstari wa 7.

Baada ya ombi lao hilo, "Musa aliwaombea watu". Na matokeo yake, Bwana akamuambia Musa:

> "…Jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi. Musa akafanya nyoka ya shaba, akaiweka juu ya mti, hata ikiwa nyoka amemwuma mtu, alipoitazama ile nyoka ya shaba, akaishi." Kitabu cha Hesabu 21:8-9

Hiki ni kitendawili cha ajabu sana! Ili waokolewe, Waisraeli walipaswa kuitazama sanamu ya kiumbe yule yule ambaye alikuwa akiwaua. Dawa pekee ya sumu ya nyoka inayoua ilikuwa ni kumtazama nyoka aliyetengenezwa kwa shaba.

Sasa hebu tuuchunguze mstari wa kuvutia kwenye Agano Jipya kuhu-

su asili ya ubinadamu wa Kristo.

> "Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi,"
> Kitabu cha Waebrania 2:14

Mwishoni mwa somo hili, tutachunguza ulinganisho unaoshangaza uliopo kati ya aya hizi mbili (Kitabu cha Waebrania 2:14 na Kitabu cha Hesabu 21:9). Ingawa kwa sasa, acha tuangalie kwa ufupi maisha ya mfalme.

Mnamo mwaka 2012, Jumba la Makumbusho la nchini Australia lilifanya maonesho ya Alexander the Great. Pale mtu alipoingia kwenye maonyesho hayo alikutana na swali lililoandikwa kwa herufi kubwa kwenye ukuta wa kuingilia kwenye jengo. Swali liliuliza hivi: 'Ni lini Alexander aliitwa mtu mkuu kwa mara ya kwanza?' Na chini ya maandishi hayo makubwa kuna jibu la kihistoria: 'Takriban miaka mia tatu baada ya kifo chake.'

Nilipolisoma swali hilo, mara moja nilikumbuka andiko la Kitabu cha Danieli 8:8. Nilikumbuka jinsi Biblia ilivyomuita Alexander 'mtu mkuu' zaidi ya miaka mia moja kabla hata yeye mwenyewe hajazaliwa. Kwa kweli, Biblia inasema alikuwa ni "mtu mkubwa sana". Na kwamba kwa nguvu zake zote—kwa uwezo wake wa juu kabisa—ukuu wake ungetwaliwa. Ungevunjwa.

Alexander alikufa akiwa na umri wa miaka 33 pekee, lakini historia inamtaja kuwa ni mmoja wa wanaume majasiri zaidi waliopata kuishi duniani. Hakuwahi kuruhusu vita vianze akiwa nyuma, bali mara kwa mara alikuwa yupo mstari wa mbele kupigana akiwaongoza askari wake kwenye hali ngumu kabisa ya kivita. Wakati fulani, Alexander alikuwa akiingia kwenye jiji lenye ngome nyingi. Askari wake walipoanza kupanda kwenye kuta, walishambuliwa na mishale mikali na mafuta ya moto. Kwa mara ya kwanza kabisa, Alexander aliwaona askari wake wakirudi nyuma huko vitani. Ila bado yeye alikuwa yupo tayari kuitumia fursa hiyo na kupambana, Alexander akabeba ngazi na kukwea

juu ya ukuta ule.

Kwa upande mwingine, hata hivyo, Alexander alizungukwa na maadui, na haikuchukua muda mrefu mpaka alipokaribia kuuawa. Hata hivyo, kwenye kushuhudia tendo hilo la kijasiri, askari wa Alexander waliorudi nyuma kwenye vita walipata nguvu mpya ya mapambano. Kwa kweli, iliwatia nguvu kwa kiwango kikubwa kiasi kwamba walisongea mbele kwa ujasiri mpya, na wao pia wakaanza kuuruka ukuta. Hatimaye, mtu mweusi anayeitwa Cleitus—ambaye alikuwa ni mshirika wa karibu wa Alexander—aliyaokoa maisha ya Alexander the Great. Huu ndio aina ya ushujaa unaotangaza jina la Alexander Mkuu.

Bila shaka, ni jina la mtu mwenye akili nyingi za kijeshi. Alexander aliweza kubadilisha mwenendo wa vita ndani ya muda mfupi sana. Aliweza kutambua udhaifu ulipo na mara moja akajua ni mbinu gani za kuzitumia. La muhimu zaidi, Alexander aliwapa hamasa wanajeshi wake. Ingawa kila mara alikaribia kuzidiwa kwa idadi, hakuwahi kupoteza vita hata mara moja. Kwenye vita vya Arbela, Alexander alizidiwa kwa idadi ya hadi askari 200,000. Na hata hivyo, bado ushindi ulikuwa wake. Kwa kweli, labda Arbela ilikuwa ni ushindi mkubwa zaidi kwa Alexander. Ushujaa wake, umahiri na ustadi wake haukuwa na kifani.

Matokeo yake, umahiri wa Alexander umeandikwa kwenye kurasa zote za historia. Hata leo, maonyesho yanafanyika ili kutunza urithi wa mshindi huyu ikiwa imepita karibu miaka 2500 baada ya kifo chake.

Unaona, Alexander aliamua kukumbukwa kila nyakati. Ilikuwa ni kutokana na tamaa hii kiasi kwamba Alexander alijijengea jiji. Wakati huo, jiji la Alexandria huko Misri lilikuwa ni jiji kuu duniani kutokana na maktaba yake, falsafa, na busara. Cha kusikitisha ni kwamba, pia lilisifika kwa kiasi kikubwa kwenye mafundisho ya kipagani na uwepo wa maandiko ya Biblia yaliyopotoshwa.

Walakini, hayo yalikuwa ni mafanikio ambayo Alexander aliyatimiza ili kukumbukwa wakati wote. Lakini swali langu kwako ni hili: Je, Alexander the Great atakumbukwa mbinguni? Fuatana nami kwenye Kitabu cha Ayubu sura ya 24.

> “Chaka na hari hukausha maji ya theluji; Kuzimu nako hao ambao wamefanya dhambi. Tumbo lililomzaa litamsahau; buu litamla na kuona tamu; Hatakumbukwa tena; Na udhalimu utavunjwa kama mti.” Kitabu cha Ayubu 24:19-20

Ayubu anasema kuwa watu waovu hawatakumbukwa mbinguni. Na ijapokuwa kwa ushindi wake wote, Alexander alikufa akiwa ni mlevi, mpotovu, na asiye na maadili; mtu jeuri. Hivi ndivyo Biblia inavyosema kuhusu watu waovu:

> “Wao wametukuzwa; lakini kitambo kidogo hutoweka; Naam, hushushwa, na kuondolewa njiani kama wengine wote, Nao hukatwa kama vile masuke ya ngano.” Kitabu cha Ayubu 24:24

Wakati wa kurudi kwa Kristo, jina la Alexander Mkuu halitakumbukwa tena. Baada ya kufa kwenye hali ya ulevi, upotevu, Alexander alipotea milele. Lakini Mkristo mnyenyekevu zaidi anayemkubali Kristo kama Mwokozi wake hataishi milele pekee, bali atakuwa na jina la milele na milele. Jina ambalo linazidi sana ukuu wa Alexander Mkuu.

Kwenye Kitabu cha Isaya 56 tunapata ahadi nzuri sana. Ni kifungu nilichowahi kumuonesha mchungaji anayeshika mafundisho ya siku ya Jumapili ambaye aliamini kuwa Sabato haina umuhimu tena. Aliniomba nimuoneshe ni wapi kwenye Biblia ambapo watu wa mataifa walitakiwa kuishika Sabato, kwa hiyo nilimpeleka kwenye maelezo ya kifungu hiki.

> “Heri afanyaye haya, na mwanadamu ayashikaye sana; azishikaye sabato asizivunje; auzuiaye mkono wake usifanye uovu wowote.” Kitabu cha Isaya 56:2

Angalia kile ambacho nabii anasema kwenye aya ifuatayo:

> “Wala mgeni, aambatanaye na BWANA, asiseme hivi, Hakika yake BWANA atanitenga na watu wake; wala towashi asiseme, Mimi ni mti mkavu.” Kitabu cha Isaya 56:3

Hapa tunapata ahadi ambayo si ya Israeli peke yake. Ahadi hii, kama ambavyo Bwana anasema, ni kwa ajili ya mtoto wa mtu mgeni. Ahadi hii inamzunguka kila mwanadamu; mtu yeyote ambaye amejiunga na Bwana. Na kwenye ahadi hii, Kristo anazungumza na towashi na kusema: “wala towashi asiseme, Mimi ni mti mkavu”.

Towashi ni mtu aliyehasiwa. Hawezi kupata watoto. Kwa hivyo, hakuna mtoto wa kuliendeleza jina la familia. Lakini Mungu anamuagiza towashi kuwa asijiangalie “kuwa yu mti mkavu”. Kinyume chake, Kristo anamhakikishia hivi:

> "Nitawapa hawa nyumbani mwangu, na ndani ya kuta zangu, kumbukumbu na jina, lililo jema kuliko kuwa na wana na binti; nitawapa jina lidumulo milele, lisilokatiliwa mbali." Kitabu cha Isaya 56:5

Ahadi hii nzuri inaendelea kwenye sura nzima. Kwenye mstari wa 7, Bwana anathibitisha kuwa: "Nitawaleta hao nao hata mlima wangu mtakatifu".

Kwa wale wanaoweka agano na Bwana na kuishi kwa utiifu kwa mapenzi yake, Mungu anaahidi jina ambalo kamwe halitatupwa. Jina litakalodumu milele yote. Kitu kile kile ambacho Alexander alikitafuta sana kinapatikana kwa mtu mpole, mnyenyekevu zaidi anayemkubali Kristo maishani mwake. Unaona sasa jinsi ilivyo, Alexander the Great alishindwa vita. Alipoteza vita kubwa zaidi ambayo inaweza kupiganwa. Vita dhidi ya nafsi/mwili.

Ndio, Alexander alipiga na kushinda sehemu kubwa ya ulimwengu unaojulikana. Hakuna jeshi au askari ambaye angeweza kusimama mbele yake. Lakini hakuweza kushinda mwili wake. Sheria ya dhambi ilimchakaza kiongozi huyu mkubwa wa majeshi. Ingawa alikuwa ni mfalme—mtawala wa ulimwengu—alikuwa kwenye utumwa wa dhambi; mtumwa wa kifo. Na umilele unapoanza, kumbukumbu yake, mambo aliyoyatimiza, na jina lake yote hayo yatasahauliwa.

Ni sawa kwa kila mmoja wetu leo hii. Bila kujali jinsi ambavyo unaweza kuwa ni mtu maarufu, tajiri kiasi gani, au mwenye kuonewa wivu kwa kiasi gani, usipoishindia nafsi yako, wewe pia utaangamia. Jina lako litatoweka, na maisha yako yatasahaulika.

Kila nafsi inahusika kwenye hii vita. Mtu yeyote anayekufa huku akitii sheria ya dhambi kwa kupenda yeye mwenyewe—akiishi ili kujifurahisha yeye mwenyewe—atapotea milele. Atakufa kwa dhambi yake, ambapo ni kufa kwenye uasi dhidi ya Mungu, sheria Yake, na serikali Yake. Kwenye hali kama hii, hakuna anayefaa kuingia kwenye ufalme wa mbingu. Vinginevyo, dhambi isingekuwa inaisha na ungekuwa ni mtu mwenye dhambi asiyeweza kufa. Kwa hiyo Bwana hana chaguo. Ni yule tu ambaye maisha yake na tabia yake imebadilishwa ndiye ambaye anaweza kuaminiwa na kuokolewa, na kuaminiwa kuingia kwenye milango iliyopambwa kwa lulu.

Mabadiliko haya ya muhimu ndiyo ambayo Biblia inaita ushuhuda wa kuzaliwa mara ya pili. Ni wokovu ulio wa kweli. Unahitaji maisha mapya, mawazo mapya, na matamanio mapya. Angalia namna ambavyo mtume Paulo anavyoelezea ushuhuda huu.

> “Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.” Kitabu cha 2 Wakorintho 5:17

Biblia inamuita mtu aliyeokolewa kuwa ni “kiumbe kipya”. Maisha ya zamani—pamoja na tabia na mazoea yake yote—yamepitwa na wakati. "Yamekuwa mapya". Fikiria jinsi ambavyo kifungu hiki kilivyo wazi. Wokovu sio marekebisho ya maisha ya zamani. Sio uboreshaji. Ni maisha mapya kabisa. Ndiyo maana ikaitwa 'kuzaliwa mara ya pili'.

Hili ni jambo la muhimu sana kwa sababu hapo ndipo wengi wananaswa. Leo hii, Wakristo huelekeza ufahamu wao wa wokovu juu ya kanisa na yale wanayoyashuhudia. Lakini ninawasihi; usiweke ufahamu wako kwenye vitu ambavyo vinakuzunguka. Weka ufahamu wako kwenye yale ambayo yameandikwa kwenye Neno la Mungu! Kitabu cha 2 Wakorintho 5:17 kinatuambia kwamba "mtu akiwa ndani ya Kristo ame-

kuwa kiumbe kipya". Utu wa kale umekwenda zake. Hautambuliki tena kwa sababu nafsi haitawali tena. Sasa, anaishi kwa kufuata sheria ya mbinguni. Ana mawazo matakatifu, nia yenye upendo, na matamanio ambayo ni safi.

Mwanzoni mwa safari yangu ya Ukristo, nilishuhudia kwa dhati tukio hili la kuzaliwa mara ya pili. Ingawa nimehangaika mara chache tangu wakati huo, ninashuhudia mbele za Mungu juu ya ushuhuda nilioupitia maishani mwangu wakati huo—kwenye maisha yangu ya maombi, kwenye maisha ya familia yangu, na kanisani. Na mimi nilikuwa ni mtu ambaye nilikuja moja kwa moja kutoka kwenye mahangaiko ya kidunia. Kama vile mtoto anayeelezewa na Paulo kwenye Kitabu cha 1 Wakorintho 13, sikujua chochote. Lakini nilipokuwa nikijifunza na kusoma, Mungu alinifunulia polepole kile nilichopaswa kukifanya, na ambacho ningekitumia maishani mwangu. Kwa haraka sana, Bwana alikuwa akinibadilisha. Hatua kwa hatua, kama vile "nilipokuwa mtu mzima, nimeyabatilisha mambo ya kitoto." Kitabu cha 1 Wakorintho 13:11.

Ila leo hii, hivi ndivyo kanisa linavyofundisha kuhusu kuzaliwa mara ya pili:

1. Mtu huisikia injili (iwe ni kwa kuambiwa, kupitia kwenye jumuiya, au kutaniko la Mungu) na kuikubali.
2. Mtu huyo anahudhuria masomo ya Biblia.
3. Anafanya marekebisho kwenye maisha yake (mabadiliko ya mtindo wa maisha, mabadiliko ya kiafya, n.k).
4. Anafikia uamuzi wa kubatizwa.
5. Anakuwa mshirika kanisani.

Kimsingi, hivi ndivyo kanisa linavyouona mchakato wa wokovu. Unaamuliwa na mambo ambayo mtu huyafanya. Hapa, bado mtu anatenda dhambi mara kwa mara na kisha anazitubu. Zaidi ya hayo, anafundishwa kuamini kuwa jambo hilo nila kawaida. Theolojia nzima kwenye kanisa inasisitiza jambo hilo. Ndiyo maana asili ya Kristo ni somo lenye utata sana kwenye kanisa la leo. Endapo asili ya Kristo ilikuwa ni tofauti na yako wewe mwenyewe kwa namna yoyote, basi unaweza tu kutenda dhambi na kutubu. Wajibu wako pekee unakuwa

ni kuendelea kuwa mtu bora.

Enyi marafiki, falsafa hii ya kuridhika siyo ile ambayo inafundishwa kwenye Biblia. Ingawa kanisa zima na kila Mkristo ulimwenguni anaweza kuwa anaishi maisha ya dhambi-na-kutubu, hiyo haifanyi jambo hili kuwa sawa. Ni lazima ufahamu wa mtu aliyeokoka uwekwe kwenye msingi wa Neno.

Kwa mara ya kwanza nilivyoanza kufundisha ushindi juu ya dhambi, nilishuhudia lawama nyingi sana. Mara nyingi, nilishutumiwa kufundisha 'ukamilifu'. Kwa kuanzia, Dada Ellen White anasema kuwa "kadri unavyomkaribia Yesu, ndivyo utakavyojiona kuwa ni mwenye makosa zaidi machoni pako; kwa maana mtazamo wako utakuwa wazi zaidi, na kutokukamilika kwako kutaonekana kwa upana na tofauti kabisa na asili Yake ambayo ni kamilifu." (Ellen G. White, *Steps to Christ*, 64.)

Jambo la pili, endapo nitashindwa kuishi maisha yangu kulingana na kile ninachokifundisha, sibadilishi neno la Mungu kutokana na jambo hilo. Silitafsiri neno la Mungu kwa njia tofauti kwa sababu hakuna mtu ulimwenguni anayepata ushindi dhidi ya dhambi. Neno la Mungu linatuambia "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu". Kitabu cha Mathayo 5:48. Amri ipo wazi kabisa. Matatizo hutokea pale tu watu wanapoweka ufahamu wao wa sheria ya Mungu kwa kuwafuata wale ambao ni wengi. Wanauweka ufahamu wao juu ya yale ambayo wanafundishwa na wanatheolojia, yale ambayo wahudumu wa kanisani wanayafundisha, na hata yale wanayoona yakitendeka mbele ya macho yao. Matokeo yake, wokovu wa Biblia unaeleweka kuwa unamaanisha maisha ya 'dhambi-na-kutubu'. Hivi ndivyo Shetani anavyotaka tuamini! Huu ni udanganyifu wake kuhusu ushuhuda wa wokovu.

Kwenye barua ya Paulo kwa Wakorintho, tuliona ufafanuzi wa kweli wa wokovu. Sasa hebu tuone jinsi mtume Yohana anavyoufafanua.

> "Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi;…" Kitabu cha 1 Yohana 3:6

Je, kuna nafasi yoyote ya kuwepo dhambi kwenye mstari huu? Vipi kwenye mstari wa 8?

"atendaye dhambi ni wa Ibilisi;…" Kitabu cha 1 Yohana 3:8

Kwa Mkristo aliyeokoka, kunatakiwa kusiwe na nafasi ya ubinafsi maishani mwake. Kusiwe na nafasi ya shetani; hakuna mahali pa maisha ya 'dhambi-na-kutubu'. Ushuhuda wa kweli wa kuzaliwa mara ya pili ni maisha ya ushindi! Kwa maana ni maisha yanayochochewa na matunda ya rohoni; matendo yanayoamuliwa na upendo, furaha, na amani.

Enyi marafiki, hivi ndivyo mtu anavyopata ufahamu wa wokovu. Unategemea Neno la Mungu, sio juu ya kile ambacho kanisa lako au mchungaji anafundisha. Neno la Mungu haliwezi kusema uongo. Na neno la Mungu linahitaji kuwa "Kila alitajaye jina la Bwana na auache uovu." Kitabu cha 2 Timotheo 2:19.

Endapo unajiita Mkristo na kulitaja jina la Kristo, unatakiwa kuwacha kabisa uovu. Unaona, wokovu si marekebisho ya mambo ya zamani; sio uboreshaji. Unaweza kurekebisha au kuboresha nyumba ili kuifanya ionekane kuwa ni bora, lakini bado nyumba ni ile ile. Hiyo siyo maana ya kuwa kiumbe kipya. Kuwa kiumbe kipya inamaanisha kubomoa kabisa nyumba ya zamani, na kuijenga kutokea kwenye msingi mpya. Msingi wa Neno Takatifu la Mungu.

Mnaona marafiki, Shetani si mjinga kiasi cha kutojua ukweli huu. Anajua nguvu ya wokovu wa kweli kwa sababu Amekuwa akiutazama kwa miaka elfu sita. Aliuona kwa Habili, Sethi, na watu watakatifu kote kwenye ukoo huo Mtakatifu. Aliuona kwa manabii, mitume, wanaofanya matengenezo ya rohoni, kwa Wakristo waliotupwa kwenye simba, na kwa wanaume na wanawake wenye msimamo wa unyenyekevu. Ameona roho zikipata ushindi wa kweli; nafsi zinazomshuhudia Kristo na zikaishi maisha yao ndani Yake. Shetani amekuwa akiutazama kwa maelfu ya miaka. Kwa hiyo mtu anapokuwa na ushuhuda huo wa uhai, Shetani anajua kuwa anapata hasara kubwa. Hiyo ndiyo sababu pekee ya yeye kuwekeza sana kwenye udanganyifu wa ushuhuda wa wokovu. Pale mtu anapoelewa wokovu wa kweli na kuutumia kwenye

maisha yake, Shetani hupoteza uwezo wake juu ya mtu huyo.

Hivyo, ametengeneza mfumo wa kudanganya. Ushuhuda wa kidini unaodanganya ambayo kanisa hufundisha kuwa ni wokovu. Kwenye mfumo huu, mtu anafundishwa kuzishika amri (barua ya sheria); kujifunza Biblia na kuifundisha kwa wengine; kukuza tabia njema; kujali mabadiliko ya kiafya; na kuwasaidia wahitaji.

Kwa sasa unaweza kuwa umechanganyikiwa kidogo. Hakuna kitu kibaya kwa kufanya lolote miongoni mwa mambo haya! Bila shaka, tunapaswa kuzishika amri. Bila shaka, ni lazima kuwe na mabadiliko ya kiafya katika maisha. Bila shaka, mtu anapaswa kusoma Biblia yake, kuwa mtoaji kwa jamii yake, na kustawisha tabia inayofaa.

Tatizo la mfumo huu, hata hivyo, ni mafundisho kuwa haya mambo yanajumuisha wokovu. Hii inasababisha mtu kuyatimiza mambo hayo kwa ulazima na kwa nguvu zake yeye mwenyewe. Hapa ndipo penye tatizo. Mkristo anaweza kuwa na nidhamu kubwa. Wanajeshi wanazoeshwa kuwa waaminifu kwenye jeshi, wanariadha wanazoeshwa kujituma kwenye michezo, na Wakristo pia wanaweza kujizoesha kuzifuata sheria za Mungu. Lakini hiyo haimaanishi kwamba wameokoka. Watu wanaweza kutunza sheria kwa maandishi, lakini hawazihifadhi mioyoni mwao. Inategemea ipi ni hamasa ya kwa nini unafanya kile unachokifanya.

Kwa hakika, miaka elfu mbili iliyopita Yesu aliona udanganyifu huu. Aliyaona mambo haya haya yakiwemo ndani ya mtu aliyeitwa Nikodemo, na akayadhihirisha. Unaona namna ilivyokuwa, Nikodemo alikuwa ni Mfarisayo; mtawala wa Wayahudi. Hakuna aliyezishika amri na sheria kama yeye alivyofanya. Alifanya mabadiliko makubwa zaidi ya kiafya. Naye hakuwa ni mwanafunzi tu au mwalimu wa Biblia; bali pia Yesu alimuita bwana wa Israeli. Alikuwa ni mtu wa hisani sana na alisaidia wenye uhitaji pamoja na kanisa. Nikodemo alikuwa na tabia isiyo na dosari. Hakuwa mnafiki. Kwa hiyo kwa sifa hizi zote, unaweza kufikiria jinsi ambavyo Nikodemo alijiona? Je, unajua jinsi wenzake walivyomtazama?

> "Alikuwa ni Mfarisayo ambaye anazifuata sana sheria, na alijivunia matendo yake mema. Aliheshimiwa sana kwa ukarimu wake na upendo wake kwenye kuendeleza huduma ya hekaluni, na alijihisi yu salama machoni pa Mungu….alijiona kuwa ana uhakika wa kuuona ufalme wa Mungu. Alijiona kuwa yeye hahitaji mabadiliko yoyote yale." (Ellen G. White, *The Desire of Ages*, 171)

Mtu huyu—kwenye maisha yake, ujuzi, na tabia—hakuwa na makosa. Hakuna mwingine zaidi ya Kristo ambaye angeweza kuyaona maisha yake kwa undani. Ingawa Nikodemo alikuwa na uhakika kuwa hahitaji mabadiliko yoyote, Yesu aliuona uhitaji wa kweli ndani yake.

> "Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Kitabu cha Yohana 3:3

Nikodemo alijiona ya kuwa alikuwa salama na kwamba ana nafasi kwenye ufalme. Lakini Bwana anamuambia mtu huyu: usipozaliwa mara ya pili, hauwezi kuuona ufalme wa Mungu.

> "Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu." Kitabu cha Yohana 3:5

Enyi marafiki, Yesu hasemi na Kayafa au mtu mwingine muovu, mpotovu. Kristo alimpata mtu mwenye tabia isiyo na dosari sana huko Yerusalemu, na anamuambia mara mbili: ni lazima uzaliwe mara ya pili ama sivyo hauwezi kuingia kwenye ufalme wa mbinguni.

Ukweli mchungu ni kuwa, leo hii Wakristo wengi wapo kwenye hali hii. Kwa hakika, Nikodemo anatuzidi sana inapokuja suala la matendo ya nje na maarifa yake, na hata kwa uaminifu. Nikodemo alidanganywa kwa sababu alikuwa akiufuata mfumo wenye udanganyifu, lakini bado alikuwa ni mwaminifu. Kwa hivyo unafikiri Kristo angesema nini kwako wewe na mimi?

Fikiria kwa muda ni kwa nini shuhuda tisa ziliandikwa. Ni ushuhuda

kwa akina kaka na dada kwenye kanisa (wazee, wahudumu wa kiroho, n.k) ambao walikuwa wanaivunja kabisa imani yao na bado walifikiri walikuwa wakitembea na Bwana. Hiyo ndiyo sababu kwa nini tunahimizwa kuzisoma. Mara nyingi mtu atayaona mambo mengi maishani mwake kupitia shuhuda hizo.

Mwisho wa siku, mzizi wa tatizo huwa ni ule ule. Yote yanategemea kama mtu ameokoka au hajaokolewa. Kila jambo la kanisani, kila mkanganyiko—iwe ni mgawanyiko au fundisho la uongo—linarudi kwenye nafsi kuwa hazijaokolewa. Ni rahisi tu kwa namna hiyo. Unapotatua tatizo hili, unatatua matatizo yote kwenye kanisa. Wakati kanisa linapokuwa limejaa wanaume na wanawake waliojiweka wakfu na waliookolewa, kuna umoja wa kiimani. Kuna imani iliyo safi. Na hakuna ubishi. Hii inawezaje kuwa hivi? Ni kwa sababu Wakristo waliookolewa kweli hawaishi kwa ajili ya nafsi zao tena. Wanaishi kwa ajili ya Kristo. Ni uamsho ambayo inapaswa kutokea kabla ya mwisho wa dunia kufika.

Sasa, kwa kweli hii ni habari njema. Hata hivyo uamsho unaweza tu kufanyika kwa wale wanaotambua hitaji la uamsho kwenye maisha yao. Unaona ilivyokuwa, Nikodemo alijiona ya kuwa hakuwa na haja ya kubadilika. Kwa hiyo uamsho unawezaje kutokea maishani mwake akiwa kwenye hali hiyo? Ndiyo maana ni kitu kinachochanganya. Ndiyo maana alidanganyika. Na ni sababu hiyo hiyo inayomfanya Kristo azungumze nasi hata leo. Inatubidi kutambua hitaji la mabadiliko kwenye maisha yetu kabla ya uamsho muhimu kutokea.

Kwa sasa unaweza kuwa unafikiria kama endapo Nikodemo alikuwa na sifa hizi zote ambazo ni nzuri na bado alipaswa kuzaliwa mara ya pili, kuna tumaini gani kwangu mimi? Rejea nami kwenye Kitabu cha Yohana sura ya 3, na uone kifungu ambacho Kristo anayaelekezea mawazo ya Nikodemo.

> “Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa;” Kitabu cha Yohana 3:14

Watu wa Israeli walipaswa kutazama ili waishi. Nikodemo alijua hasa

kile ambacho Kristo alikuwa akikiongelea aliporejelea ushuhuda huu. Angalia mstari wa karibu yake ambao unafuatia.

> "ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye." Kitabu cha Yohana 3:15

Waisraeli walipaswa kuamini kwa imani kwenye nyoka ambaye aliinuliwa juu ya mti. Walijua kuwa hakukuwa na thamani ya kuokolewa kwenye sanamu hiyo ya shaba, lakini imani yao ilipaswa kupenya hadi kwa Masihi, Mwokozi wao. Nikodemo alilielewa jambo hili kikamilifu. Na Yesu akamuambia kuwa nyoka aliyeinuliwa ni unabii unaomuonesha yeye mwenyewe. Kwa jambo hili, Yesu alikuwa akisema hivi: 'Ninyi mnapaswa kunitazama ili mpate wokovu. Usifikirie kuwa umekubaliwa kwa huruma za Mungu. Unatazama mahali pasipofaa. Usiangalie kazi zako, sifa zako, wasifu wako. Umeumwa na nyoka na unahitaji kuokolewa na sumu mbaya. Nitazame mimi ili uishi.'

Kazi ya wokovu—kazi ya Roho Mtakatifu—ni kazi isiyo ya kawaida. Ilimbidi Nikodemo atafute nguvu za Kiungu. Mtu anaweza kupanga kuhudhuria mafundisho ya Biblia, kwenda kanisani, na kubatizwa. Lakini mtu hawezi kupanga kuzaliwa mara ya pili. Kwa nini? Kwa sababu hiyo siyo kazi inayoanzishwa na mwanadamu. Kazi hiyo inaanzishwa na Mungu. Mwanadamu anatakiwa kuitikia wito wa Mungu. Hapaswi kupinga.

Roho Mtakatifu anapofanya kazi juu ya moyo wako, anapoyachochea mawazo matakatifu ndani yako, matamanio, na mabadiliko, na unapoanza kuyatafakari mambo haya na kuvutwa kwenda kwa Kristo, ushuhuda wa kuzaliwa mara ya pili huanza. Na ingawa haupaswi kuupinga, ni Mungu ndiye anayeianzisha kazi hiyo. Haina uhusiano wowote na mwanadamu. Ndiyo maana Kristo anamuambia Nikodemo: inakupasa kuzaliwa kutoka juu. Ndiyo maana Anasema hivi:

> "Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho." Kitabu cha Yohana 3:8

Kwa ujumla, ni kazi inayomilikiwa na Mungu. Sisi tunachotakiwa kukifanya ni kuitikia tu wito wake na sio kupingana Naye. Hivi ndivyo Nikodemo alivyopaswa kufanya. Hivi ndivyo Kristo anavyotuvuta kwenda kwake Yeye; kama ilivyoelezewa kwenye Kitabu cha Yohana 3:14. Na Yesu anaurudia ujumbe huu kwenye Kitabu cha Yohana 12:32.

> "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu." Kitabu cha Yohana 12:32

Ni ahadi nzuri. Hata kama tutashindwa kushiriki kwenye injili, Kristo anaahidi kuwa Yeye, akiwa pale msalabani, atawavuta watu wote kwenda kwake. Kila mwanadamu atavutwa Kwake. Haijalishi kama wewe ni Muislamu, Mhindu, mtu usiyemuamini Mungu, mtu usiyeamini uwepo wa Mungu, au kama ni wa vuguvugu wa karne mpya. Haijalishi wewe ni mtu wa dini au historia gani. Unaweza kuwa Mueskimo, au mzaliwa wa kutoka kwenye eneo la mbali ambalo hakuna mmisionari aliyewahi kufika huko, lakini Kristo anasema kwamba atawavuta watu wote kwenda Kwake. Anafanya hivi kwa kupitia Roho Wake, akitenda kazi kwenye dhamira ya mtu. Kwa hakika kila mtu amepewa ujuzi wa mema na mabaya. Na kwa Roho wa Kristo, akitenda kazi juu ya dhamira zao, Anatafuta namna ya kuwavuta kwenda Kwake.

Sababu iliyomfanya Nikodemo atakiwe kuzaliwa mara ya pili ni kwa sababu alipokuwa akimtii Mungu, alikuwa akifanya hivyo kwa ulazima. Leo hii, watu wengi kwenye kanisa wanafanya mambo mazuri kwa sababu hiyo hiyo. Hilo ndilo jambo linalokuza uhusiano huu wa 'dhambi na kutubu'. Mwanadamu anajaribu kumtii Mungu kwa nguvu zake yeye mwenyewe, kwa hivyo wakati mwingine anashindwa kumtii. Hiyo inaitwa kazi. Nia siyo sahihi. Ngoja nikuoneshe mfano.

> SWALI: Ni kwa nini watu wengi huenda kazini?

> JIBU: Kutokana na ulazima wa kufanya hivi.

Watu wanatakiwa kulipia matumizi yao, wanahitaji chakula. Hatimaye, wana mahitaji. Lakini ni nini hufanyika wakati watu wanaposhinda bahati nasibu kubwa? Je, ni jambo gani la kwanza wanalolifanya kwa

ujumla? Wanaacha kufanya kazi. Kwa sasa mahitaji yao yanatimizwa. Watu hufanya kazi kwa sababu ya mahitaji yao.

Nikodemo alifanya kazi ya kujitahidi kufika mbinguni. Hitaji lake ilikuwa ni kwenda mbinguni. Nia yake ilikuwa ni ya ubinafsi. Yesu alimuonyesha kwamba nia yake ilikuwa sio sahihi. Ndiyo maana ilimbidi azaliwe mara ya pili.

Unaona ilivyokuwa, unaweza kufanya mambo mengi mazuri na bado ukawa na ubinafsi. Nikodemo alifanya mambo mengi mazuri, lakini yalifanywa kwa nia isiyo sahihi. Biblia inasema hivi:

> "Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu." Kitabu cha 1 Wakorintho 13:3

Unapomtendea mtu jambo fulani kutokana na upendo, hautarajii chochote kutoka kwake. Kitabu cha Mwanzo kinaeleza "Yakobo akatumika miaka saba kwa kumpata Raheli. Ikawa machoni pake kama siku chache tu kwa vile alivyompenda." Kitabu cha Mwanzo 29:20. Kwenye kitabu cha Warumi, Paulo anasema hivi:

> "Kwa maana ningeweza kuomba mimi mwenyewe niharimishwe na kutengwa na Kristo kwa ajili ya ndugu zangu, jamaa zangu kwa jinsi ya mwili," Kitabu cha Warumi 9:3

Watu wa ukoo ambao Paulo anawataja hapa walikuwa ni Wayahudi waliomchukia. Kwa nia na madhumuni yote, walikuwa ni maadui zake wakubwa. Hata hivyo Paulo anatamani kwamba yeye angeweza kukataliwa kuingia kwenye mbingu ya milele ili tu wao waokolewe. Je, hapo zawadi yake ni ipi? Je, malipo yake ni yapi? Hakuna zawadi. Hakuna malipo. Anafanya hivyo kutokana na upendo.

Ni kwa nini wazazi wenye upendo huwafanyia watoto wao mambo mazuri? Je, watoto huwa wanawalipa wazazi? Je, watoto wanaweza kuwalipa? Je, kwa nini wazazi hutoa dhabihu? Kwa nini wanakosa mahitaji yao wao kwa muda mrefu ili tu watoto wao wapate kula na ku-

vaa? Je, kwa nini mke mwenye upendo anamfanyia mumewe mambo mazuri na mume anamfanyia mke wake mambo mema? Ili kulipwa? Hapana, wanafanya hivyo kutokana na upendo.

Ninaye mama mkubwa anayekaa nchini Italia ambaye ana umri wa zaidi ya miaka themanini. Kamwe hakuwahi kuolewa. Alikuwa ni binti mwenye mvuto sana na mwenye haiba nzuri. Hakuolewa kwa sababu alijitolea maisha yake yote kumtunza mama yake, nyanya yangu. Mama yake alikufa akiwa na umri wa miaka 99, na mama mkubwa alimtunza nyanya yangu maisha yake yote. Alijitolea kila kitu ili kumtunza mama yake. Na alimtunza hadi pumzi yake ya mwisho. Hakukuwa na hospitali, hakukuwa na huduma ya uuguzi. Akawa anambeba, anamuogesha, na alikuwa akimlisha. Na alifanya hivyo hadi pumzi ya mwisho ya mama yake kwa furaha kabisa.

Miaka kadhaa iliyopita, mama yangu alikwenda nchini Italia kumsaidia ili apumzike. Na mama yangu hakuwa mzembe. Wanawake wachache walifanya kazi kwa bidii kama yeye kwenye maisha yake. Lakini hakuweza kufanya kile ambacho dada yake alikifanya. Mama yangu alikuwa akitokwa na machozi wakati alipokuwa akizungumza juu ya upendo aliokuwa nao dada yake kwa ajili ya mama yake. Hiyo ni huduma inayotokana na upendo. Haisubiri malipo yoyote.

Nikodemo alipaswa kugeuzwa kutoka kwenye kumtumikia Mungu kwa ulazima, hadi kumtumikia kwa shukrani. Je, unafahamu namna ilivyokuwa? Kupitia Kitabu cha Yohana 3:14.

> “Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa;” Kitabu cha Yohana 3:14
>
> "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu." Kitabu cha Yohana 12:32

Nikodemo alipomuona Yesu pale Kalvari, alivutwa Kwake. Tangu wakati huo, Nikodemo hakuwa mtu yule yule. Alikuwa amemshuhudia Mwana wa Mungu akitundikwa msalabani. Alikuwa ameona Muumba

wa ulimwengu wote mzima akifa kwa ajili yake. Na makusudio yake yote yalibadilishwa.

Mara nyingi tunakinukuu Kitabu cha Yohana 3:16, lakini tukisoma kwenye muktadha wa mazungumzo haya, kina nguvu sana. Kumbuka, mazungumzo kati ya Yesu na Nikodemo yalianza na kauli ya Nikodemo:

> "Huyo alimjia usiku, akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye." Kitabu cha Yohana 3:2

Kwa hivyo, Yesu anapoyasema maneno kwenye Kitabu cha Yohana 3:16, anamuambia Nikodemo: 'Mimi si Rabi fulani tu. Mimi si mwalimu mkuu. Mimi ndiye Mwana pekee wa Mungu.'

> "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Kitabu cha Yohana 3:16

Nikodemo alimuona Mwana wa Mungu akifa kwa ajili yake na kufa kwa ajili ya ulimwengu. Na alitambua kuwa kazi zake zote nzuri zisingeweza kumuokoa. Alikumbuka maneno ya Yesu usiku ule takriban miaka mitatu iliyopita. Alikumbuka ahadi ya Yesu kuwa "ili kila mtu amwaminiye asipotee". Na hapo ndipo Uthibitisho wa Biblia unasema, Nikodemo aliona hitaji lake la muokozi.

> "Aliona kuwa utii pekee wa sheria ulio mgumu zaidi kama unavyotumika kwa ajili ya maisha ya duniani usingeweza kumpa mtu yeyote haki ya kuuona ufalme wa mbinguni." (Ellen G. White, *The Desire of Ages*, 174)

Ni kwa nini Nikodemo alitambua hitaji lake pale msalabani? Kwa sababu ya unabii uliotolewa kwenye Kitabu cha Yohana 3:14.

> "Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo

hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa;" Kitabu cha Yohana 3:14

Fikiria tena maisha ya Alexander the Great. Hakuna jeshi au mpiganaji wa kijeshi ambaye angeweza kumuua. Kilichomuua ni dhambi. Alexander aliendelea kuitii sheria hiyo ya nafsi hadi mwisho wake, alikuwa amelewa sana hata akanyongwa na matapishi yake mwenyewe hadi akafa. Alikuwa mtu mpotovu na asiye na maadili. Tamaa zake hazikumtosheleza. Alexander the Great alikufa akiwa mateka kabisa.

Bado haina maana endapo ni mtu asiye na maadili kwa nje au mtu aliye na muonekano wa tabia isiyo na dosari. Kama Nikodemo asingevutwa kwa Kristo pale msalabani, yeye pia angepotea. Bwana aliwaita Waandishi na Mafarisayo kuwa ni "makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote." Kitabu cha Mathayo 23:27

Ona jinsi ilivyo, nyoka anapokung'ata, kinachokuua sio kile kitendo cha kung'atwa bali ni ile sumu anayoiingiza. Kwa bahati mbaya, Australia ina nyoka waliopo kwenye nafasi nne za juu duniani kwa kuwa na sumu kali zaidi. Na nyoka mbaya zaidi duniani anaitwa Inland Taipan. Sumu yake ni kubwa sana kiasi kwamba ikiwa utang'atwa na Inland Taipan na usipopata msaada, basi ni hakika kuwa baada ya saa chache utakuwa umekufa. Bila ya muujiza wa Mungu hauwezi kuokolewa. Hivi ndivyo nyoka huyu alivyokuwa na sumu.

Sasa, unaweza kuwa unashangaa ni kwa nini nyoka ambaye ni kiumbe mbaya alitumiwa kama ishara ya Kristo. Ili ulielewe jambo hili, unapaswa kwanza uelewe namna tiba ya kung'atwa na nyoka inavyopatikana.

Dawa ya sumu ya nyoka ni kinga ya sumu, ambayo hutoka kwenye nyoka. Sumu hukamuliwa kutoka kwenye nyoka na kisha hudungwa ili iingie kwenye farasi mwenye afya kwa kuwekewa dozi ndogo ndogo. Muda huo huo farasi hutengeneza kingamwili ili kuzuia sumu. Kisha, damu hutolewa kutoka kwenye farasi, husafishwa, na kudungwa kwa yule aliyeathirika. Sasa una dawa ya kukinga sumu iliyotengenezwa kutoka kwenye sumu. Na hiyo ndiyo inayokuponya. Kitu ambacho ki-

likuwa kinakuua sasa kinakuwa ndiyo njia ya kuyaokoa maisha yako.

Ilikuwa ni sheria ya dhambi iliyomuua Alexander, na ambayo itatuua pia kama hatutajisalimisha. Hii ni sumu ya nyoka. Ni sheria ya dhambi. Mara tu unapoingia kwenye ulimwengu huu unakuwa chini ya sheria hiyo. Ina maana nafsi hiyo inataka kutawala. Kwa hiyo njia pekee ambayo Kristo angeweza kukuokoa na sumu hii ni kuwa chini ya sumu ile ile Kwake Yeye mwenyewe. Ilimpasa Awekwe chini ya sheria hiyo ya dhambi kwenye mwili; wenye dhambi, kwa asili ya roho iliyoanguka ambayo chini yake kila nafsi huzaliwa duniani. Kisha, Kristo alilazimika kuitakasa kwa kuishi maisha yaliyo matakatifu na kamwe hakuiruhusu dhambi itawale. Na kwa hivyo alitengeneza ile dawa ya kujikinga na sumu. Kinga ya sumu kwa ajili ya dhambi ni sheria ya Roho.

Ingawa Kristo alidungwa sumu ya dhambi (asili ya dhambi) hata mara moja Hakuwahi kudhurika na hiyo sumu. Inawezekanaje ikawa hivyo? Ni kwa sababu asili sio dhambi! Hauna haja ya kufundisha hali ya usafi. Hautakiwi hata kuibadili asili ya Kristo kwa sababu asili si dhambi. Kristo alidungwa kwa sumu ile ile tunayoirithi. Je, ni kwa namna gani tena angetengeneza kinga za mwili kwa ajili ya hiyo sumu? Je, anawezaje kukusaidia kama hakushiriki kwenye kile ulichokuwa nacho? Kristo alirithi asili yetu ya kuanguka na dhambi zetu. Lakini hata mara moja Yeye hakuwahi kuathiriwa nazo. Aliziangamiza. Aliziangamiza lini? Pale juu msalabani.

> "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu." Kitabu cha Yohana 12:32

Yesu alipaswa kuishi maisha yaliyo matakatifu kwa miaka thelathini na tatu na nusu. Hata pale msalabani, angeweza kufanya dhambi. Ilimbidi afe kwa imani. Alichukua asili ya dhambi iliyoanguka msalabani, na akaitakasa asili hiyo. Aliyasafisha maisha hayo na kuiondoa sumu ya dhambi. Na hivyo alijenga kingamwili kamilifu dhidi ya sumu. Bwana Yesu alitoka kaburini akiwa ametukuzwa. Ndiyo maana dhambi haitakiwi tena kumshikilia Mkristo. Dhambi imeshindwa. Kinga ya sumu imetengenezwa.

Kristo alipaswa kuichukua sehemu ya mwili na damu yetu. Ilimbidi kuichukua sehemu yetu ya asili ile ile yenye dhambi, sumu ile ile iliyokuwa ikiwaua watu wa Israeli. Ilimpasa kuishiriki kwenye hili jambo ili kuendeleza upinzani dhidi yake.

Rejea nami kwenye Kitabu cha Waebrania 2:14 pale tulipoanzia mwanzo.

> "Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi," Kitabu cha Waebrania 2:14

Nguvu ya Shetani juu yetu ni sheria ya dhambi, inayotambulika wakati mtu anapotenda dhambi. Na dhambi hupelekea kifo (Kitabu cha 1 Wakorintho 15:56). Kristo alitakiwa kushiriki kwenye sheria hiyo ili kuiharibu. Hata hivyo hakuitenda hata mara moja. Kamwe hakufanya dhambi hata mara moja. Angalia huu mstari unaofuatia.

> "awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa." Kitabu cha Waebrania 2:15

Hivyo ndivyo Kristo anavyotukomboa kutoka kwenye dhambi. Baada ya kushiriki kwenye asili yetu, na kuibeba sumu ile ile, Yesu aliyastawisha maisha makamilifu. Ndiyo maana Biblia inazungumza sana kuhusu damu ya Kristo. Fikiria mifano hii minne.

> "…Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake," Kitabu cha Ufunuo 1:5

> "basi si zaidi damu yake Kristo,… itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?" Kitabu cha Waebrania 9:14

> "…na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote." Kitabu cha 1 Yohana 1:7

> "Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango." Kitabu cha Waebrania 13:12

Damu ya Kristo inao uwezo wa kutusafisha kutokana na matendo maovu kama ilivyokuwa kwa Nikodemo. Inatuosha na dhambi zetu na kututakasa. Damu ya Kristo (maisha Yake yaliyo kamili) imebeba kinga.

Kwenye Kitabu cha Yohana sura ya 6, Kristo alihubiri ambapo alisema kuwa Yeye alikuwa mkate wa uzima, na ambaye atauila mwili wake na kunywa damu yake atauona uzima wa milele. Hata hivyo, karibu kanisa nzima ilikataa. Wakasema hivi: "Neno hili ni gumu, ni nani awezaye kulisikia?" Kitabu cha Yohana 6:60. Lakini walijua kile ambacho Yesu alikuwa akikisema. Ni kwamba tu hawakuwa tayari kuishi maisha ambayo Aliyaishi; maisha ya kujitoa nafsi yake sadaka.

Mara nyingi hatukitambui kile tunachokishiriki pale tunaposhiriki kwenye ibada ya ushirika mtakatifu (meza ya Bwana). Ndiyo maana unaweza kujiingiza kwenye hukumu kwa kushiriki kwa namna isivyostahili. Kwa maana unaposhiriki ibada ya ushirika mtakatifu, unashiriki uzima wa Kristo. Na maisha ya Kristo ni maisha ya umaskini na kujitoa nafsi sadaka. Ni maisha ambapo Mwana wa Adamu hakuwa na mahali pa kukilaza kichwa chake ili kupumzika. Kwa hiyo, watu wanashiriki ushirika mtakatifu lakini hawataki kushiriki kwenye uzima Wake. Ndiyo maana wanaondoka kama namna ambavyo hawa ndugu walifanya. Mara kwa mara Yesu alikuwa akiwaambia hivi:

> "…Amin, amin, nawaambieni, Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu, hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake." Kitabu cha Yohana 6:53-56

Ni lazima mkristo ashiriki kwenye maisha ya Kristo kwa ukamilifu na kwa utimilifu kwa sababu Yeye pekee ndiye anayeweza kuwasafisha

kutoka kwenye dhambi; kutoka kwenye sumu ya nyoka. Kama mtume Paulo anavyosema kwamba:

> "Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, je! Si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo?" Kitabu cha 1 Wakorintho 10:16

Ndiyo maana kuna nguvu kwenye huduma ya ushirika inapoeleweka kwa usahihi. Kwa kushiriki kula mkate na kuinywa divai, unaukubali ushindi wa Kristo kama ni wako wewe mwenyewe. Unashiriki kuinywa damu yake ambayo imeshinda sheria ya dhambi, na ambayo humsafisha mtu dhidi ya dhambi! Maisha hayo matakatifu aliyoyaishi Yesu yanakuwa ni ya kwako. Kwenye damu ya Kristo, unapokea ushindi dhidi ya dhambi.

Wakati wa matengenezo ya kanisa, huduma ya ushirika ilikuwa ni moja ya mambo yaliyoleta mabishano makubwa. Hii ni kwa sababu Shetani anajua kuwa ibada ya ushirika inapoeleweka kwa usahihi na kutekelezwa, kutakuwa na uamsho mkubwa sana. Ndiyo maana imekuwa ikipotoshwa kwa muda mrefu.

Tukirejea kwenye kichwa cha ujumbe wetu, Sister White anaeleza ni kwa nini sanamu ya nyoka mwenye mauti ilichaguliwa ili kumuwakilisha Kristo.

> "Watu walitambua vyema kuwa nyoka mwenyewe hakuwa na uwezo wa kuwaokoa. Ilikuwa ni ishara ya Kristo. Kama vile sanamu iliyofanywa kwa mfano wa nyoka wanaoangamiza ilivyoinuliwa kwa ajili ya uponyaji wao, ndivyo Yule aliyefanywa "mfano wa mwili ulio wa dhambi" angekuwa ndiye Rehema yao. Kitabu cha Warumi 8:3." (Ellen G. White, *The Desire of Ages*, 175)

Ni ukweli mzuri ulioje ambao tumejifunza! Ukweli ambao haujaeleweka vyema kwa zaidi ya miaka elfu mbili. Ni Uthibitisho wa Biblia pekee ambao ungeweza kutufunulia somo halisi la kuinuliwa kwa yule nyoka wa shaba. Sister White anaunganisha Kitabu cha Hesabu 21:8-9 na Kitabu cha Warumi 8:3. Ile "sanamu iliyofanywa kwa mfano wa nyoka

waharibifu" ilikuwa ni mfano wa "Mwili ulio wa dhambi'"!

Enyi marafiki hapa mnaona jinsi ilivyo, si kweli kuwa wale nyoka wenye sumu ndiyo waliokuwa wakiwaua watu kule nyikani. Ilikuwa ni dhambi zao. Nyoka walikuwa ni matokeo tu ya uasi wa Waisraeli. Uponyaji wao ungeweza kufanyika kwa kupata tiba ya dhambi zao tu. Walipaswa kumtazama kwa imani Yule "aliyefanyika kwa sura ya mwili wenye dhambi". Ndiye pekee aliyekuwa na kinga ya dhambi zao. Hii ndiyo sababu Sister White anaunganisha Kitabu cha Hesabu 21:8-9 na Kitabu cha Warumi 8:3.

Waisraeli walipokuwa wakimtazama nyoka kwa imani, walikuwa wakimtazama Kristo. Na kwa hivyo tunapaswa kumuangalia kwa imani Yule anayeweza kutupatia ushindi juu ya dhambi, tukiwa tumeshiriki naye kwenye ugonjwa wetu huo huo (asili ya dhambi), na bado tukaishi maisha ya ushindi na kulishinda kaburi na mashirika yote ya kishetani. Ni nyoka aliyepigiliwa misumari pale msalabani. Ilikuwa ni sheria ya dhambi ambayo ilihukumiwa hapo.

> "Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili;" Kitabu cha Warumi 8:3.

Kamwe sheria isingeweza kutoa haki ambayo ilitakiwa iwe sababu ya udhaifu wa mwili; sheria ya dhambi. Lakini Mungu alimtuma Mwanawe akiwa kwenye mwili huo huo ulioanguka. Naye alifanya nini? Aliilaani dhambi kwenye mwili!

Ndiyo maana anatuamuru tukule mwili Wake na kushiriki kuinywa damu Yake. Damu Yake imetakaswa, na inatiwa kwetu kwa imani. Tunapotazama ili tuishi, tunajua kuwa Yeye anayo kinga ya dhambi zetu. Hivyo ndivyo Nikodemo alivyopaswa kufanya. Ilimbidi aache kuzitazama kazi zake, kwenye kanisa, na kwa watu wote waliokuwa wakimsifu kwa namna alivyokuwa akifanya vyema. Biblia inasema kuwa uchungu unaoleta kifo ni dhambi. Kitabu cha 1 Wakorintho 15:56. Lakini mstari

unaofuata unasema hivi: "Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo". Kitabu cha 1 Wakorintho 15:57.

Baada ya kusimulia hadithi ya Nikodemo kwenye sura ya 17 ya kitabu cha *The Desire of Ages*, Sister White anauliza swali lifuatalo:

> "Je, sasa, tunaokolewa kwa namna gani? "Kama vile Musa alivyomuinua juu yule nyoka kule jangwani," ndivyo Mwana wa Adamu alivyoinuliwa, na kila mtu ambaye amedanganywa na kung'atwa na nyoka anaweza kumtazama na kuishi. "Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" Kitabu cha Yohana 1:29. Nuru inayoangaza kutoka msalabani inadhihirisha upendo wa Mungu. Upendo Wake unatuvuta kwenda kwake Yeye. Endapo tutakubali kuvutwa kwenda Kwake, tutaongozwa kuelekea pale msalabani kwa ajili ya toba ya dhambi ambazo zimemsulubisha Mwokozi. Kisha Roho wa Mungu kwa njia ya imani huyazalisha maisha mapya kwenye nafsi. Mawazo na matamanio yanatii mapenzi ya Kristo. Moyo, akili, zinaumbwa upya kwa mfano wake Yeye atendaye kazi ndani yetu ili kuvitiisha vitu vyote kwake Yeye. Kisha sheria ya Mungu inaandikwa kwenye akili na moyo, na tunaweza kusema hivi pamoja na Kristo, "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu;" Kitabu cha Zaburi 40:8. (Ellen G. White, *The Desire of Ages*, 175)

Jina la Nikodemo linamaanisha 'ushindi wa watu'. Pale Nikodemo alipomuona Kristo akifa kwa ajili yake, hakumuona tu Yule ambaye alikufa kwa ajili ya dhambi zake bali Yule ambaye angeweza kumuokoa kutoka kwenye dhambi zake. Nikodemo alivutwa kwake, na wakati huu, hakupinga.

> "Upendo Wake unatuvuta kwenda kwake Yeye. Endapo tutakubali kuvutwa kwenda Kwake, tutaongozwa kuelekea pale msalabani kwa ajili ya toba ya dhambi ambazo zimemsulubisha Mwokozi. Kisha Roho wa Mungu kwa njia ya imani huyazalisha maisha mapya kwenye nafsi." (Ellen G. White, *The Desire of Ages*, 175)

Hiki ndicho kilichotokea kwa Nikodemo. Utajiri wake wote, ujuzi wake

wote, muda wake wote, vilikuwa vimewekwa wakfu tena kwa utumishi wa Mungu. Lakini wakati huu, haikuwa inafanyika kwa ulazima. Wakati huu, ilitokana na upendo. Nikodemo hana budi kuishi na kufa kwa ajili ya jambo moja, nalo lilikuwa ni Kristo. Kwa kweli, *The Desire of Ages* inasema kuwa alikuwa na imani kuu zaidi kuliko wanafunzi. Kwa maana pale msalabani wote walitilia shaka, lakini Nikodemo hakuwa na shaka. Pale msalabani Nikodemo alijua Yesu alikuwa ni nani hasa. Alikumbuka mazungumzo yao. Alikumbuka maneno ya Kristo; tazama ili uishi.

Hebu waza kuwa uko peke yako jangwani, ukiwa umeng'atwa na nyoka mwenye sumu kali sana. Ghafla, mtu anafika ambaye ana kinga ya sumu hiyo. Anakukaribia na kutaka kukupa matibabu ya kung'atwa na nyoka. Utafanya nini? Utataka ujue sayansi iliyotumika kutengeneza kinga hiyo ya sumu wakati unaangamia? Hakika jibu ni hapana. Bila ya kusitasita, utaomba dawa hiyo iingizwe kwenye damu yako haraka iwezekanavyo.

Sister White anapozungumza kuhusu Musa kumuinua juu nyoka akiwa kule nyikani, anatuonya tusiulize kuhusu jinsi ambavyo Roho Mtakatifu anafanya kazi, kuhusu sayansi ya hayo yote. Hatuwezi kuelewa mambo haya. Tunachotakiwa kufanya ni kutazama tu ili tuishi. Kuamini kuwa Yesu ana dawa ya matatizo yetu, na kutazama yale yote aliyotufanyia. Halafu tunatakiwa kuipeleka imani pale msalabani. Kwa kuwa huko, hautataka tena kuishi kwa ajili yako wewe binafsi. Hapo, utamtumikia kwa upendo, na kazi zako zote zitakuwa na maana. Wakati huo, sisi—kama watu binafsi na kama kanisa—tunaushuhudia wokovu kama vile Nikodemo alivyoupata, ulimwengu utashuhudia 'ushindi kwa ajili ya wanadamu'.

*"Musa akafanya nyoka ya shaba, akaiweka juu ya mti, hata ikiwa nyoka amemwuma mtu, alipoitaz ma ile nyoka ya shaba, akaishi."*
*Kitabu cha Hesabu 21:9*

## Je, nini maana ya kuokolewa?
## Je, Yesu alikuwa na asili gani hapa Duniani?
## Je, ninawezaje kushiriki kwenye maisha ya Kristo?

Kwenye kitabu cha Hesabu kuna hadithi ya kweli yenye kuvutia kuhusu nyoka ya shaba. Iliyoandikwa na Musa, hadithi hii ina somo ambalo halikueleweka kabisa mpaka ilipopita miaka elfu moja na mia tano baada ya kutokea; wakati wa mazungumzo ya faragha kati ya Yesu na Nikodemo.

Leo hii, miaka mingine elfu mbili baada ya mahojiano yaliyofanyika jioni hiyo, tunakwenda kujifunza ukweli mwingine mzuri kutoka kwenye hadithi hii ya ajabu ya kinabii.

EARTHEN VESSELS
2 CORINTHIANS 4:7